THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2 **Ijumaa, 15 Oktoba 2010 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali yote.
3. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 8 zenye maandishi.

Scanned by CamScanner

SEHEMU A: (Alama 10)
SUNNAH NA HADITH

1. Chagua jibu sahihi katika maswali (i) – (x) kisha uandike herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia,

(i) Maelezo yanayotoa maana ya Sunnah kiutendaji ni
- A Sunnah ni mila ya maisha ya Mtume (s.a.w)
- B Sunnah ni mwenendo wa Mtume (s.a.w)
- C Sunnah ni mapokezi kutoka kwa Mtume (s.a.w)
- D Sunnah ni yale aliyoyafanya Mtume (s.a.w)
- E Sunnah ni ibada za ziada alizofanya Mtume (s.a.w).

(ii) Utayatambua vipi maelezo yaliyoko mbele yako kuwa ni hadithi ?
- A Maelezo hayo yawe kwa lugha ya Kiarabu.
- B Maelezo yawe na Isnad na Nabawiyyi.
- C Maelezo yawe na Matin na Isnad.
- D Maelezo yawe na Matin na Riwaya.
- E Maelezo yawe na wapokezi watatu au zaidi.

(iii) Kazi kubwa ya kwanza ya uandishi wa hadithi iliyofanywa na swahaba wa Mtume (s.a.w) ilikuwa ya
- A Abubakar Swidiq (r.a)
- B Malik bin Anas.
- C Uthman bin Affan (r.a)
- D Bukhar na Muslim
- E Ally bin Abii Twalib (r.a).

(iv) Uandishi wa hadithi sahihi ulifikia kilele chake katika kipindi cha
- A Tabii Tabiina
- B Maswahaba
- C Mtume (s.a.w)
- D Makhalifa wanne wa mtume (s.a.w)
- E Tabiin.

(v) *Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala msijiepushe naye na hali mnasikia. (8:20)*
Kwa mujibu wa aya hii, waumini
- A hawana budi kumsikiliza Mtume (s.a.w).
- B wanatakiwa kumuiga Mtume (s.a.w) katika kuendesha maisha yao ya kila siku.
- C wanatakiwa kuzisoma na kuzihifadhi hadithi za Mtume (s.a.w).
- D ni lazima kufuata Sunnah ya Mtume katika maisha yao ya kila siku
- E hawana budi kufuata Qur'an na Sunnah kwani ndiyo dalili ya Uislamu wao.

Scanned by CamScanner

(vi) Sababu ya kutoshamiri uandishi wa hadithi wakati wa Mtume (s.a.w) ni
A Mtume alikuwepo hivyo allwapa waumini kila walichohitaji katika kutekeleza Uislamu.
B Mtume aliwakataza kuandika hadithi ingawa baadaye aliwaruhusu.
C Dola ya Kiislamu ilikuwa ndogo na hapakuwa na ugumu wa kuwasiliana.
D Waislamu walishughulika zaidi na uandishi wa Qur'an.
E waumini walishughulishwa na kuuhami Uislamu dhidi ya maadui.

(vii) Hadithi ina sehemu kuu mbili; Isnad na Matin. Isnad inawakilisha
A wasimulizi wa hadithi waliomsikia au kumuona Mtume.
B wasimulizi wa hadithi kuanzia kwa Mtume hadi kwa aliyeipokea.
C wasimulizi mashuhuri wa hadithi za Mtume.
D aliyeandika hadithi katika kitabu pamoja na wasimulizi.
E wasimulizi wadhibitifu wanne au zaidi.

(viii) Tukio kubwa lililoongeza kasi ya ukusanyaji wa hadithi katika vitabu ni
A kupanuka Dola ya Kiislamu hadi Hispania.
B kupatikana kwa vituo vya hadithi vya kutosha.
C kukusanywa kwa Qur'an wakati wa Khalifa Uthman (r.a).
D Khalifa Ali (r.a) kufikishwa mahakamani na Myahudi kujibu shitaka.
E kugundulika karatasi wakati wa Umar (r.a).

(ix) Hadith sahihi inatakiwa ifikie kigezo kifuatacho:
A Wapokezi wake wawe wadhibitifu
B Ikidhi vigezo vya hadithi sahihi
C Isimzuie Mtume (s.a.w)
D Iwe katika Bukhar au Muslim
E Iwe na Isnad na Matin.

(x) Hadithi nyingi ziliandikwa katika karne ya
A tano hijiriya
B pili hijiriya
C kwanza hijiriya
D tatu hijiriya
E nne hijiriya.

Scanned by CamScanner

SEHEMU B: (Alama 15)
QUR-AN

2. Chagua kutoka **orodha B** kifungu cha maneno kinachowiana na kifungu cha maneno kutoka **orodha A**. Vifungu vya orodha B vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

ORODHA A:

(i) Na (Mtume) akamuona (Jibrili) mara nyingine (kwa sura yake ile ile ya Kimalaika katika usiku wa miiraji). (53:13)

(ii) Na wanapokutana na walioamini husema: "Tumeamini"; na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao husema: "Hakika sisi tu-pamoja nanyi, tunawacheza shere tu." (2:14)

(iii) Mtume (s.a.w) amesema: "Kutafuta elimu ni faradhi kwa Muislamu mwanamume na Muislamu mwanamke."

(iv) Na katika watu, wako wasemao: "Tumemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho"; na hali ya kuwa wao si wenye kuamini." (2:8)

(v) "Na namna hii Tumemfanyia kila Nabii maadui; (nao ni) mashetani katika watu na (mashetani katika) majini." (6:112)

(vi) "Sisi hatukusikia haya (ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja hata) katika hii mila ya mwisho. Hayakuwa haya (ya kusema Mungu ni Mmoja tu) ila uzushi (tu)." (38:7)

(vii) Basi kwa hakika pamoja na dhiki (huja) faraji. Hakika pamoja na dhiki (huja) faraji. (94 :5-6)

(viii) Basi naapa kwa mnavyoviona na msivyoviona, kwa hakika hii ni kauli iliyoletwa na Mjumbe (wa Mwenyezi Mungu) mwenye heshima (kubwa). (69:38-40)

(ix) Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika mwangaza. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni mashetani. Huwatoa katika mwangaza na kuwaingiza katika giza. (2:257)

(x) (Shetani) anawaahidi (mambo ambayo hayatakuwa), na anawatumainisha (ambayo hawatayapata); kwani shetani hawaahidi ila udanganyifu tu. (4:120)

(xi) Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao; nao hawatambui. (2:9)

(xii) .... Sema: "Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?" Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu. (39:9)

(xiii) Ametukuka Mwenyezi Mungu. Mfalme wa haki. Wala usiifanyie haraka (hii) Qur'an (kwa kusoma), kabla haujamalizika Wahyi (ufunuo) wake. Na uombe useme: "Mola wangu, nizidishie elimu." (20:114)

(xiv) Na huzungumzi (Muhammad) kwa matamanio ya nafsi yake. Isipokuwa (anayoyazungumza ni) Wahyi uliofunuliwa kwake" (53:3).

(xv) Ewe Mtume! Mbona unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu! (66:1).

Scanned by CamScanner

ORODHA B:

A Qur'an ni ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
B Allah huongoza watu katika nuru na shetani huwapeleka watu katika giza
C Wanafiki.
D Madai ya makafiri dhidi ya Qur'an wakati wa Mtume (s.a.w).
E Kutafuta elimu ni amri.

SEHEMU C: (Alama 15)
TAWHIID

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Aya ya Qur'an (2:285) inataja nguzo za Imani kama ifuatavyo:
(i) Wote wamemwamini Mwenyezi Mungu, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake na Mitume Yake;
(ii) Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na Waislamu, (pia wameamini hayo):
(iii) (nao hao Waislamu na Mtume wao) husema: "Hatutofautishi baina ya yeyote katika Mitume Yake (wote tunawaamini)."
(iv) (Tunakuomba) msamaha, Mola wetu! Na marejeo ni kwako."
(v) Na husema: "Tumesikia na tunatii.

(b) (i) Katika Uislamu imani juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu si suala la Kibubusa.
(ii) Mwanadamu ametunukiwa akili na milango ya fahamu iii kutafakari juu ya alama (ishara) mbalimbali kuthibitisha kuwepo kwa Allah (s.w).
(iii) Kumkanusha Mwenyezi Mungu kunakwenda sambamba na kukanusha ufufuo.
(iv) Pamoja na miujiza waliyoonesha Mitume, kuna alama nyingine nyingi zilizotajwa katika Qur'an zinazothibitisha kuwepo Mwenyezi Mungu.
(v) Miongoni mwa hoja kubwa za wakanao ufufuo ni kuwa ni mahali mtu hufufuka baada ya kuoza na mifupa yake kusagika sagika.

(c) Mtazamo wa Qur'an juu ya Dini ni kama ifuatavyo
(i) Kwa hiyo, kwa mtazamo halisi wa Qur'an ukafiri nao ni dini kwani Mungu si lazima awe Mungu muumba.
(ii) Mtazamo wa Uislamu juu ya dini ni tofauti kabisa na ule wa kikafiri.
(iii) Katika Qur'an tunafahamishwa: "Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu...." (9:31).

Scanned by CamScanner

(iv) Qur'an na historia vinathibitisha kuwa mwanadamu hajawahi kushindwa kukabiliana na mazingira yake jambo linalodhoofisha hoja ya makafiri kuwa mwanadamu alianza maisha akiwa mjinga.

(v) Katika Qur'an, Dini imeelezwa kama utaratibu wa maisha tofauti na tafsiri iliyomo katika kamusi kuwa Dini ni mambo ya kiroho juu ya Mungu muumba na kuwa Dini imetokana na uduni wa mawazo ya mwanadamu.

SEHEMU D: (Alama 30)
FIQH

4. Jibu kwa ufupi kwa kujaza nafasi zilizo wazi katika swali la (i) – (xv). Andika neno au maneno yanayokosekana tu katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Mwenyezi Mungu amemkusudia mwanadamu kuwa (a) _____ wake hapa ulimwenguni na nyenzo itakayomuwezesha kufikia cheo hiki ni (b) _____.

(ii) (a) _____ ndio kiingilio cha Uislamu ambacho ni kusema (b) _____.

(iii) Dharura za kutoswali swala ya faradhi kwa wakati wake ni (a) _____ au (b) _____ kwa mwanamke.

(iv) Rakaa moja ya swala itahesabiwa kuwa imekamilika iwapo nguzo zake zote zimekamilika. Nguzo hizo zimegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni (a) _____ na (b) _____.

(v) Katika Qur'an (2 :264) Mwenyezi Mungu anatukataza waumini tusiharibu Sadaka zetu kwa kuzifuatilia kwa (a) _____ na vile tunavyotoa viwe vya (b) _____.

(vi) Watu waliotajwa katika Qur'an kuwa wanastahiki kupewa zakat kutokana na dharura ya ugumu wa maisha ni (a) _____ na (b) _____.

(vii) Makosa mawili ambayo Muislamu akiyatenda anawajibika kufunga miezi miwili mfululizo ni (a) _____ na (b) _____.

(viii) Sunnah zilizoambatana na funga ya Ramadhani ni pamoja na (a) swala ya tarawehe (b) kufuturu mapema, (c) _____ (d) kutafuta usiku wa Laitlatul Qadir na (e) _____.

(ix) Miezi ya kunuia Hija ni (a) shawal (b) _____ na (c) _____.

(x) Matendo yanayofanywa na mwenye kuhiji siku ya mwezi 10 Dhul Hija pale Mina ni (a) _____ (b) _____ na (c) kunyoa nywele au kupunguza.

(xi) Kwa mujibu wa Qur'an, Muislamu anawajibika kuchuma mali kwa njia za halali na kujiepusha na tabia ya kufanyia (a) _____ na kutoitumia kwa (b) _____.

(xii) Katika sheria ya familia ya Kiislamu wanaume na wanawake ambao ni haramu kuoana wanajulikana kwa jina la (a) _____ na mtu anayeozesha huitwa (b) _____.

Scanned by CamScanner

(xiii) Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umaskini. Sisi ndio tunaowaruzuku wao na nyinyi (pia) (17:31). Msimamo wa Uislamu juu ya kampeni ya kudhibiti uzazi ni (a) _____ kwa kuwa swala la riziki liko kwa (b) _____.

(xiv) Ila wale wenye kuamini na kutenda mema, watakuwa na ujira usiokwisha (unaoendelea maisha) (95:6). Msingi mkuu wa maadili katika Uislamu ni (a) _____ na kuwa jambo jema au ovu hutegemea maamrisho au makatazo ya (b) _____.

(xv) Katika nchi inayoongozwa Kiislamu, mamlaka yote ni ya (a) _____. Sheria au kanuni za msigi za maisha ya Waislamu hutokana na (b) _____.

SEHEMU E: (Alama 30)
TAREKH

Chagua **neno** au **kifungu cha maneno** (i) – (xxx) ili ukamilishe kauli (a) – (p) kwa usahihi.

Maneno au vifungu vya maneno

(i) Peponi
(ii) Moto
(iii) Toba haraka
(iv) Kutakabari
(v) Adam
(vi) Yaghuutha
(vii) Kwa siri
(viii) Ibrahim (a.s)
(ix) Nuhu (a.s)
(x) Muhammad (s.a.w)
(xi) Safa
(xii) Kumhonga Mtume (s.a.w)
(xiii) Yathrib
(xiv) Badr
(xv) Umar bin Abdul-Aziz
(xvi) Udongo
(xvii) Ibilisi
(xviii) Idris (a.s)
(xix) Yauqa
(xx) Kwa uwazi
(xxi) Umar bin Khattab
(xxii) Kosa lake
(xxiii) Hunain
(xxiv) Suhail bin Amr
(xxv) Kumlaghai Mtume (s.a.w)
(xxvi) Walimwengu wote
(xxvii) Musa (a.s)
(xxviii) Adam (a.s) na Hawa
(xxix) Ismaili (a.s)
(xxx) Abuu Lahab

Maswali

(a) _____ walianza maisha yao _____.
(b) Ibilisi alikataa kumsujudia Adam kwa kuwa yeye ameumbwa kwa _____ na Adam ameumbwa kwa _____.
(c) Mtu bora katika wakosaji ni yule anayeleta _____ baada ya kugundua _____ kama walivyofanya baba yetu Adam na Hawa.
(d) Mtu muovu katika wakosaji ni yule anayezidi _____ badala ya kuleta toba kama alivyofanya _____.
(e) Katika Mitume waliotajwa katika Qur'an baada ya Nabii Adam ni _____ kisha alifuata Nabii _____.

Scanned by CamScanner

(f) _____ na _____ ni miongoni mwa Miungu iliyoabudiwa na watu wa Nuhu (a.s).

(g) Nabii Nuhu (a.s) alilingania watu wake kwa _____ na _____.

(h) _____ na _____ walishirikiana kunyanyua kuta za Al-Ka'abah.

(i) Watu wa Nabii _____ waliangamizwa kwa mafuriko na wale wa Nabii _____ waliangamizwa kwa kuzamishwa baharini.

(j) _____ ni katika kizazi cha Nabii Ibrahim (a.s) kupitia kabila la Quraysh na ametumwa kwa _____.

(k) Mtume (s.a.w) alianza kulingania Uislamu kwa wazi katika kilima cha _____ ambapo ami yake _____ alimuapiza.

(l) _____ na _____ ni miongoni mwa mbinu walizotumia Makafiri wa Makka kutaka kuzima nuru ya Uislamu.

(m) Mikataba ya Aqabah ilifungwa baina ya Mtume (s.a.w) na watu wa _____ ambapo ule wa Hudaibiya ulifungwa baina ya Mtume (s.a.w) na _____ kwa niaba ya Maquraysh.

(n) Mwenyezi Mungu aliwasaidia waumini katika vita vya _____ na _____ kwa kile kitendo cha Mtume (s.a.w) kupuliza udongo ulioathiri maadui na kuletewa Malaika wanaopigana kweli kweli.

(o) _____ ameitwa "Umar wa pili" kwa kuwa aliongoza kwa uadilifu kama alivyofanya _____ Khalifa wa pili wa Mtume (s.a.w).

uk print

Scanned by CamScanner